UNATAKA RAFIKI? KUWA RAFIKI!

MWONGOZO WA KUTUNZA WANYAMA NA KUEPUKA KUUMWA

Kimetengezwa na:
René Grobler, Amanda Klette,
Netcare Trauma Division
Daniel Stewart & Terence Scott
Global Alliance for Rabies Control

Translations by Pwani
Animal Welfare Org. Msa,Kenya

NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE

LUGHA YA MBWA

MBWA WANGU ANANIAMBIA NINI?

Chonjo

Shauku

Mchecheto

Ametishwa

Amekasirika

Mwenye urafiki

Anahitaji nafasi

Mimi ni Kipenzi chako
(Anapojilaza na kusugua tumbo)

Mwenye Furaha



Anachunguza

"Jambo, Nakupenda"
(Kwa salamu za kujinyoosha)

"Mimi ni rafiki yako"
(anachezesha kiuno)

"Tayari kucheza!"

"Utanilisha Chakula"

Mwenye furaha kupindukia

© 2011 Lili Chin www.doggiedrawings.net

NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE

Jinsi ambavyo watoto HAWAPASWI kujumuika na mbwa.

Ni rahisi, fikiria tu jinsi binadamu wanavyofaa kujumuika pamoja.

Epuka kuchukua chakula cha wengine.

Epuka kusumbua mbwa wakati wanapokula.

Usiibe vidude vya kuchezea kutoka kwa wenzako.

Usichukue mfupa wa mbwa au vidude vyake vya kuchezea.

Epuka kuusogeza uso wako karibu na uso wa mwenzako.

Epuka kuusogeza uso wako karibu na uso wa mbwa.

Usimsumbue mwenzako akiwa amelala.

Epuka kusumbua wanyama wakati wamepumzika. Acha mbwa aliyelala alale tu.

Epuka kusababisha kero kwa wenzako.

Epuka kumvuta mbwa mkia au masikio.

Epuka kumkanyaga au kumrukia mwenzako

Epuka kukanyaga au kumdandia mbwa.

Epuka kuwafinya wenzako.

Epuka kukumbatia. Mbwa wengi huwa hawapendi.

Epuka kufoka au kupiga nduru.

Epuka kupiga kelele pamoja na kelele zingine. km. Kupiga king'ora, ngoma nk.

Picha imechukuliwa kutoka kwa maandishi ya Dr. Sophia Yin www.drsophiayin.com

NETCARE You're in safe hands

GARC RABIES ALLIANCE

Paka rangi ndani!



NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE

UWAJIBIKAJI KATIKA UMILIKI WA WANYAMA

MAMBO 5 HURU

Ni jukumu letu kuhakikisha kila mnyama yuko na:

1. Chakula bora pamoja na maji safi.

2. Nyumba na mapumziko mazuri.

3. Matibabu anapokuwa mgonjwa au kujeruhiwa.

4. Uwepo wa wanyama wengine rafiki na wenye afya wa kucheza nao.

5. Furaha! Tunafaa kuhakikisha wanyama wetu hawashtuki wala kukasirika.

NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE

USIMUAMSHE MBWA ALIYELALA

Kuwa mcheshi na ujenge urafiki na mnyama wako!

Ni jukumu kubwa na heshima kuwa na mnyama wa kufuga nyumbani. Mnyama wako ni sehemu ya familia yako kama vile kaka au dadako. Jenga urafiki na wanyama wako na uzungumze nao.

Wanaweza kuwa marafiki wako wa dhati, na pia ni wazuri katika kuhifadhi siri. Unafaa kuonyesha heshima kwa wanyama wako wote, kama vile tu unavyowaheshimu kakako, dadako, wazazi na waalimu wako.

Ikiwezekana, tafuta chuo cha kuwafunza mbwa kinachoweza kumfunza mbwa wako kanuni za kimsingi.

Ukitaka Rafiki, kuwa Rafiki!

NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE

CHAKULA BORA NA MAJI SALAMA

Wanyama wote, kama vile tu sisi, wanahitaji chakula bora kilicho na virutubishi vyote, vitamini na madini ya Calcium, Protini, pamoja na mazuri yote tunayoyapatikana katika vyakula vyetu.

Vyakula ambavyo hatupaswi kuwapatia wanyama wetu;

NDIO	HAPANA
Nyama iliyopikwa ✓	Chokoleti x
Kuku ✓	Zabibu x
Samaki-Kiboma ✓	Vitunguu x
Mboga za Majani ✓	Kahawa x
Nafaka ✓	Kitunguu Saumu x
Viazi Tamu ✓	Premende za Kutafuna x
	Pombe x

MAHITAJI YA KIMSINGI YA KIAFYA

Kila mnyama anaweza kuugua, lakini tunaweza kuzuia jambo hili!

Wanyama wanahitaji: **Kupewa chanjo kila mwaka.**

Kunyweshwa au kulishwa dawa kila mwezi.

Kupelekwa kwa daktari wa wanyama angalau mara moja kwa mwaka.

Kupanga uzazi kwa njia ya kuwavunja kizazi wanyama wetu pia ni muhimu. Hii itasaidia kuwazuia kuzaa watoto zaidi ambao hawatapata matunzo bora.

NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE

TAFUTA NENO

D	K	U	H	E	M	A	X	V	W	O	M	D	M	F
M	P	E	P	E	R	U	S	H	A	A	N	A	T	A
P	V	C	L	N	E	P	O	M	J	H	Y	K	O	M
I	B	T	W	I	Q	W	X	A	G	I	A	T	T	I
R	T	E	M	B	E	Y	A	N	Z	K	M	A	O	L
A	S	Q	A	V	J	I	L	Y	B	N	A	R	W	I
G	J	R	K	P	H	W	R	O	O	U	W	I	A	A
V	N	Y	U	T	E	V	D	Y	S	L	A	W	M	T
I	W	T	F	E	N	U	S	A	T	G	K	A	B	Y
D	Q	F	U	J	O	M	B	W	A	E	U	W	W	K
U	H	E	N	T	K	P	T	R	B	W	F	A	A	I
D	M	W	G	I	M	K	I	A	G	Q	U	N	J	M
E	C	X	A	Y	H	N	J	K	I	W	G	Y	N	B
B	W	E	K	A	F	U	M	Y	O	E	A	A	Q	I
P	E	N	Z	I	O	S	D	F	L	R	Z	M	Z	A
M	F	U	P	A	G	V	B	N	S	A	X	A	U	L

BWEKA
CHEZA
DAKTARI WA WANYAMA
FAMILIA
KIMBIA
KUFUNGA
KUHEMA
MANYOYA
MBWA
MKIA
MNYAMA WA KUFUGA
MPIRA
MTOTO WA MBWA
NUSA
NYUTE
PENZI
PEPERUSHA
TEMBEA
VIDUDE

NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE

KUZUIA NI BORA KULIKO TIBA

"ZUIA KUUMWA KABLA HAIJAFANYIKA"

Mbwa huwa hawaelewi iwapo kuuma mtu ni makosa. Mara nyingi mbwa huuma mtu iwapo wametishwa au wanapojaribu kujikinga Ili kujizuia kuumwa na mbwa, tunafaa kuelewa:

- Jinsi mbwa wanavyohisi.
- Jinsi ya kumkaribia mbwa kwa njia salama.
- Wakati salama na usio salama wa kumkabili au kujumuika na mbwa.

Tunapoelewa tabia za mbwa na kuzuia matukio ya hatari, tunaweza kuepuka kuumwa.

ISHARA ZA HATARI

- MWILI KUSHTUKA
- MKIA KUSIMAMA WIMA
- MASIKIO YALIYOSOGEZWA NYUMA
- KURUDI NYUMA
- KUNGURUMA
- KUTOA SAUTI YA UKALI
- KUTAZAMA MUDA MREFU WA KHOFU
- MANYOYA YALIYOSIMAMA.

JINISI YA KUFANYA ✓

- WEKA MIKONO YAKO WIMA KWA MWILI
- SIMAMA WIMA NA KIMYA.

USIFANYE ✗

- USIKIMBIE
- USIPIGE NDURU AU KUWA NA WASIWASI
- MTAZAME KWENYE MACHO

KAMA UMEUMWA

- USIJIVUTE KWA NGUVU KUTOKA KWA MBWA
- BAKIA PAPO HAPO KWA MAKINI
- UKIANGUKA, JIGEUZE KAMA MPIRA HUKU MIKONO NA MIGUU UKIIWEKA PAMOJA KWA NDANI YA MWILI.

NETCARE
You're in safe hands
GARC RABIES ALLIANCE

KUZUIA KUUMWA

Tunawezaje kuzuia kuumwa na mbwa?

Mbwa tunaowajua:

Watoto wa mbwa wanapokuwa wadogo tunafaa kucheza nao mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa hawaogopi watu. Watoto wa mbwa wanafaa kufurahia kucheza na watu ili wazowee binadamu na kuepuka kuumwa. Hivyo ndivyo tunavyojenga mazowea na wanyama wetu.

Wamiliki wote wa wanyama wanafaa kujifunza jinsi ya kuwasiliana na mbwa wao, ili waweze kuepuka hali ya hatari na pia kuwafunza mbwa wao kuwa na adabu mbele za watu.

Vunja kizazi cha mbwa wako. Mbwa wa kiume ambao hawajavunjwa kizazi wanaweza kuwa wakali sana dhidi ya wanyama wengine na pia binadamu. Mbwa wa kike wanaweza kuugua wasipovunjwa Uzazi. Unapokosa kuwavunja kizazi wanyama wako inaweza kusababisha hatari kwa binadamu na pia mbwa wengine.

Mbwa tusiowajua:

Iwapo mbwa atakufuata mbio, simama wima na unyamaze kimya. Muache akunuse na anapoondoka unafaa kutembea pole pole na kimya kuelea upande mwingine.

Kaa mbali na mbwa usiyemjua. Hii inajumuisha mbwa waliofungwa minyororo au waliozungushiwa uzio.

Usiwachokoze, kuwafukuza au kurusha kitu chochote kwa mbwa. Usiwasumbue mbwa wanaokula, kulala au wanaolisha watoto wao.

Kuwa makini katika mazingira uliyopo pamoja na mbwa wanaoishi eneo hilo. Jenga urafiki na mbwa na uheshimu nafasi yao.

Usiwagonge, kuwapiga mateke au kuwafokea mbwa na pia hakikisha unakaa mbali na mbwa wanaoonyesha tabia zisizo za kawaida.

You're in safe hands

RABIES ALLIANCE

KICHAA CHA MBWA

Kichaa ni nini?

Kichaa husababishwa na virusi vinavyoathiri aina Fulani ya Wanyama lakini huathiri zaidi mbwa. Virusi hivyo hupatikana kwenye mate ya mnyama aliyeathirika, vinaweza kuingia kwa mnyama mwingine au binadamu mwenye afya kupitia kuuma au kuramba mikwaruzo na vidonda vilivyo wazi. Virusi hivyo vinaweza kusababisha kifo iwapo mgonjwa hatashughulikiwa haraka.

Tunaweza kuzuia maradhi haya hatari kwa kuhakikisha tunawapatia wanyama wetu chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa.

Epuka kuumwa

Epuka mbwa wanaozurura Ovyo.

Epuka mbwa wanaokuramba au kukwaruza.

JE, KICHAA KINAWEZA KUTIBIWA?

Lazima tujaribu kuzuia kichaa kwa kutumia chanjo! Punde tu dalili za kichaa zinapojitokeza,haiwezekani kutibu.

Kuna hatua 3 rahisi za kuzuia kichaa:

1. Kuepuka kuumwa na mnyama yeyote.
2. Iwapo umeumwa, osha kidonda kwa haraka kwa maji yanayotiririka na sabuni kwa dakika 15.
3. Mueleze mtu mzima kuwa umeumwa kwa sababu unafaa kupelekwa katika zahanati au hospitali kwa chanjo ya kichaa cha mbwa.

KUMBUKA:

Iwapo hautafaulu kumpata mtu mzima karibu nawe, hakikisha umeandamana na rafiki yako kwa sababu ni muhimu sana uweze kupata msaada.

NETCARE You're in safe hands

GARC RABIES ALLIANCE

Kwa maswali au maelezo ya kichaa cha mbwa: www.rabiesalliance.org

Gundua utofauti!

(Ziko 13)





You're in safe hands

RABIES ALLIANCE

KUZUIA KICHAA!

Iwapo umeumwa na mbwa – Osha kidonda na uelekee katika zahanati

Jinsi ya kuepuka kuumwa na mbwa!

- ✗ Kaa mbali na mbwa USIOWAFAHAMU!
- ✗ Kaa mbali na mbwa wenye tabia zisizo za kawaida – Wanaweza kukuuma!
- ✗ Usiwafukuze, kuwapiga mateke au wenye watoto wadogo!
- ✗ Usiwasumbue mbwa wanaokula, kulala au wenye watoto wadogo!

agriculture, environmental affairs & rural development

Concept by: D. Stewart Rabies Project   Designed by D.Cooke Department of Agriculture, Environmental Affairs & Rural development: Veterinary Epidemiology Section 033 3476267

NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE

HONGERA

Cheti hiki kimekabidhiwa:

____

kwa sababu najua jinsi ya kujiweka salama nikiwa na mbwa!

Naahidi ya kwamba:

- **Nitauliza ushauri kila ninapotaka kufuga mbwa.**
- **Nitaweka uso wangu mbali na uso wa mbwa.**
- **Nitasimama “kama mti” au “kama jabali” iwapo mbwa**
- **mkali atanisogelea karibu.**
- **Sitasumbua mbwa anapokula, kulala au anapokuwa na watoto.**

NETCARE
You're in safe hands

GARC
RABIES ALLIANCE